# Edeni ya Shetani

Jeffersonville, Indiana USA

Agosti 29, 1965

1 Hebu tuinamishe. Mungu mpenzi, tunakushukuru kwa nafasi hii nzuri sana ya kuja tena katika Jina la Bwana Yesu, kumkabili adui wetu; adui Wako huku kwenye uwanja wa mapambano tukiwa na Neno ili kumfukuzia mbali toka miongoni mwa watu Wako, ili waweze kuona usiku huu, Bwana, Nuru ya Injili. Ninaomba ya kwamba utayapaka macho yetu dawa hiyo ya macho, kusudi yapate kufunguliwa kwa Kweli; ili kwamba tuondoke hapa, tukisema mioyoni mwetu, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu alipokuwa akisema nasi njiani?" Waponye wagonjwa na wanaoteseka. Watie moyo waliovunjika moyo. Inua mikono dhaifu ambayo wakati mmoja ilining'inia chini. Jalia tutazame kule Kuja kwa Bwana Yesu, ambako tunaamini kumekaribia. Tunaomba hili katika Jina la Yesu. Amina.

Ketini.

2 Nitajaribu kufupisha usiku wa leo, kwa sababu najua wengi wamekuja kutoka sehemu mbalimbali za nchi, kwa ... ibada; au wamebaki humu, baadhi yenu, na yawapasa murudi mpate labda njia ya kurudi. Nami nawashukuru. Asubuhi ya leo nilitaka kumsikia Ndugu Neville, mimi mwenyewe. Nimemsikiliza mara nyingi, na sijamsikiliza hata wakati mmoja, bila kumpenda. Lakini asubuhi hii, ujumbe ule uliokuja kwa wakati uliofaa, najua mimi nilikuwa na uongozi wa Bwana kuusikiliza asubuhi hii. Mzuri sana! Nami ninaona ni kwa nini ninyi watu mnapenda kuja na kumsikiliza, pia. Na yeye siku zote atawafaa, nina hakika, kumsikiliza.

3 Nilikuwa nikijaribu kupata baadhi ya mahojiano yangu leo; asubuhi ya leo na alasiri hii. Bado nimebakiza watu wengi, wengi, wengi wa kuwaendea. Nami …

Na kama ninavyoamini ilikuwa Yethro aliyemwambia Musa wakati mmoja, akasema, "Kazi ni kubwa sana kwako." Kwa hivyo, tunao ndugu wengi sana hapa kwa ajili ya matatizo yenu. Na kila moja ya hayo ni halisi, na ni mambo mazuri yanayopaswa kushughulikiwa. Na ningewashauri mumwendee mchungaji wetu au ndugu Mann, na wahudumu wengine wa imani yetu hapa , mwaweza kuwaendea. Mnaweza kuwaendea. Wangewaambia sawa kabisa jambo la kutenda; baadhi ya watu, watoto wao; kuoana, au mambo mabaya. Na watu hawa wanaweza kukusaidia wewe tu kama—kama mtu mwingine yeyote, maana wao ni watumishi wa Kristo. Na uende kwao, nami nina hakika wata—watakupa msaada unaohitaji. Siwezi kuwafikia wote. Kuna wengi tu, kila mahali uendapo. Wanaendelea kujilimbikiza zaidi na zaidi, mnaona. Na—na unataka kumfikia kila mmoja wao, bali huwezi kufanya hivyo. Lakini ninaomba wakati wote kwamba Mungu, kwa namna fulani, ataliweka lote sawa kwa ajili yako.

4 Sasa, usiku wa leo, tunataka kuyaendea Maandiko, na kusoma sehemu ya Maandiko kutoka Mwanzo, sura ya 3; na kurejea tu nyuma kidogo kwenye baadhi ya mambo ambayo tumekuwa tukiyazungumzia katika nyakati zilizopita, na kuona kwamba Bwana Yesu atatupa cha zaidi kidogo tupate kujua tutakapoondoka. Ninaomba—naomba ya kwamba Yeye atafanya hivyo.

> *Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?*
>
> *Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula;*
>
> *Lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa.*
>
> *Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa;*
>
> *Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.*
>
> *Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala.*
>
> *Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo.*

5 Bwana na aongeze ninii … Baraka Zake katika kusomwa kwa Neno Lake. Sasa ningependa kuchukua somo usiku wa leo, kutoka kwenye hilo, na kuita: Edeni ya Shetani. Jambo dogo ghafi sana la kusema, la, *Edeni ya Shetani.* Kwa namna fulani inalingana, katika Jumapili nyingine usiku, naamini, wakati nilipokuwa nikizungumza nanyi hapa kuhusu *Chujio la Mtu Mwenye Busara*, na ladha ya mtu mtakatifu.

Na wakati mwingine maneno haya madogo madogo yanatuleta kwenye kitu fulani; linatufanya tujifunze, na kukufanya usome Neno. Na hivyo ndivyo ninavyotaka kusanyiko langu lote lifanye. "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Kwa hiyo, soma Neno;

lisome. Na msome kwa macho ya Mungu, kuwapa akili zenu ufahamu wa jinsi tunavyopaswa kuishi katika siku hii ya sasa.

6 Sasa kuja hapa, usiku wa leo, kuzungumza tu nanyi, kusema, "Vema, ningeweza kufanya *hili* ama *lile*, …"

Ninapenda kuzungumza na watu, kadiri ningetaka hata kwenda nyumbani na kila mmoja wenu usiku wa leo. Mimi … Mungu anajua hiyo ni kweli. Ningetaka kwenda nyumbani na kila mmoja wenu, na—na kula—kula kiamshakinywa pamoja nanyi asubuhi, na—na—na kwenda nje na kuwinda kindi pamoja nanyi kesho alasiri, mnaona. Ni—ningetaka kufanya jambo hilo, bali si—siwezi kufanya hivyo. Nami ningetaka kwenda nyumbani na kuketi tu na kuzungumza nanyi; niketi barazani baada ya ibada, na kuzungumza nanyi kwa muda mfupi, kuzungumza nanyi juu ya ustawi wenu na juu ya Mungu. Ningependa kufanya hivyo. Wanaume na wanawake humu ndani; Mungu anajua ningetaka kufanya hivyo, bali siwezi kufanya hivyo. Mnaona, kuna tu kama—kama mvuto na uchuvu mwingi wa akili.

7 Na—na katika wakati huu wa wasiwasi ambao tunaishi katika ... Na mimi mwenyewe ni mtu mwenye wasiwasi. Leo, nimeamua kitu fulani, "Sina budi kufanya hivyo," na kesho kiko mamilioni ya maili mbali nami; na kitu fulani kimeingilia na kufanya hili na lile. Nanyi mna wakati mgumu, kujaribu kuweka mawazo yanu sawasawa.

8 Lakini mafanikio yangu makuu ni kuhubiri Injili kupitia kwa Kanisa, na kufanya yote niwezayo kumletea Yesu Kristo heshima katika siku hii, wakati nikiwa hapa duniani, na ni wakati gani niliosalia nao duniani. Nimekuja ku—kujaribu kuwaambia jambo fulani ambalo lingewasaidia; kitu fulani. Nilisoma baada ya kwenda nyumbani asubuhi ya leo. "Ningesema nini usiku wa leo, Bwana, ambalo lingewasaidia watu hao?"

Nikisikiliza ujumbe huo wenye nguvu asubuhi hii juu ya … Ndugu Neville alituletea, karibu … Nilifikiria ulikuwa wa ajabu sana, jinsi alivyosema hapo, "Daktari ataugundua ugonjwa; lakini mtu yule anayekuja na kikarai kilichojaa sindano, hudunga sindano;" Kwa hiyo nilifikiri hilo lilikuwa kweli ni—ni dhana nzuri sana. Nilifikiria kuhusu hilo, "dawa ile ya sindano, baada ya ugonjwa kutambulika. Kwa hiyo hilo ni jambo zuri sana.

9 Nilitaka kuwaambia jambo fulani, kuwaletea kitu fulani cha kuwaangazia ahadi ya Mungu kwa ajili ya wakati huu. Mnaona? Kitu fulani, si kitu ambacho mtu mwingine alikuwa katika siku nyingine, bali kitu fulani … na wakati … Mambo hayo ni sawa; sisi sote hurejea kwenye mambo hayo. Lakini nilifikiri ningejaribu kuwaletea jambo fulani mawazoni mwenu, kwa Maandiko haya niliyoandika hapa, ambayo yangewaangazia, kujua, kuwafanya askari bora katika uwanja mnaopigania ndani sasa; kujifunza mbinu za adui, ili kwamba mweze kuzuia kila kitu kabla hakijawafikia, mnaona. Hilo ndilo jambo muhimu: ni kujifunza kujikinga na ma—makonde kadri mwezavyo.

10 Sasa, hebu na tuangalie sasa hii kubwa … kwa dakika chache, siku hii kuu, yenye dhambi tunayoishi sasa. Siamini kuna siku ambayo nimewahi kusoma katika historia … Kumekuwepo na wakati mkubwa zaidi wa mateso wakati ambapo wana wa Mungu waliuawa kila upande. Lakini kuona udanganyifu wa adui, hatujawahi kuwa na siku kama hii tunayoishi sasa. Ni siku ya ujanja sana, ya udanganyifu. Na ninapoona hilo, huniletea hili, kwamba, Mkristo anapaswa kuwa mwangalifu zaidi siku ya leo kuliko alivyowahi kuwa katika wakati mwingine wo wote.

11 Sasa, huko nyuma katika siku za mateso ya Rumi kwa kanisa, Mkristo akifanya kosa, alikwenda kwenye uwanja wa michezo, na alilishwa simba au kitu kama hicho, wakati walipompata kuwa Mkristo kwa ajili ya ushuhuda wake. Lakini nafsi yake iliokolewa, kwa sababu alikuwa msafi, mwamini asiyeghoshiwa katika Mungu na kwa furaha alitia muhuri ushuhuda wake kwa damu yake Wakati mishipa yake ilipoachilia, au matundu katika mwili wake, yalipoachilia na damu ikatiririka, angepaza sauti, kwa imani ya kweli na ya uaminifu, na kusema, "Pokea roho yangu, Bwana Yesu."

12 Lakini, sasa, ujanja wa Ibilisi sasa, unawafanya watu waamini ya kwamba wao ni Wakristo wakati si Wakristo. Hilo ndilo jambo. Si lazima uweke muhuri … Ni siku yenye hila sana kuliko vile ingelikuwa ambapo ilikulazimu kutia muhuri uhai wa—wako kwa ushuhuda wako. Ibilisi ameweka kila mtego wa ujanja awezao, ku … Yeye ni mdanganyifu. Na Yesu alituambia katika Mathayo 24 jinsi ambavyo siku hii ingekuwa ambamo tunaishi, siku ya udanganyifu sana iliyowahi kuwepo, "karibu sana kwamba ingewadanganya wale walioteuliwa na Mungu kama ingewezekana kwa yeye kudanganya."

13 Sasa hebu na tulinganishe baadhi ya Maandiko, ama unabii unaonenwa katika Biblia, kwa ajili ya siku hizi, na kuulinganisha na siku tunayoishi sasa.

Katika Timotheo wa Pili 3, tunajifunza jambo hili, ya kwamba nabii alisema, ya kwamba, "Ingekuwa katika siku hizi, ya kwamba watu watakuwa wagumu, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu." Linganisha hilo sasa, kwa muda kidogo tu. Hatutaninii … Tutayaelezea kwa kifupi, kwa sababu hatuna wakati mwingi wa kuyapitia yote kama tunavyopaswa kuyachukua; bali ni kuliangazia tu, ili kwamba uweze kuona unapofika nyumbani na kulisoma. Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko

kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, (wasiojizuia) na wasiopenda mema. "Sasa Roho alinena waziwazi ya kwamba mambo haya yatakuwa katika siku za mwisho." Hiyo ni siku hizi, unabii ukinena juu yake.

14 Sasa tunasoma, pia, katika Ufunuo … 14, Ufunuo 3:14, hasa, Wakati wa Kanisa la Laodikia, jinsi ambavyo kanisa lingekuwa katika siku hii ya mwisho. Na ingekuwa, inasema, "Yeye angeketi kama mjane wala hatahitaji cho chote. Na ingekuwa, unasema "Lingekaa kama mjane na asiwe na haja ya kitu. Li—lilikuwa tajiri, na limejitajirisha katika mali, na halijui kwamba wao walikuwa ni maskini, wenye mashaka, wanyonge, vipofu, na uchi, na hawakujua." Ninii … Sasa, kumbukeni, Yeye anazungumza na kanisa la wakati huu, "wanyonge, vipofu, uchi, wala hawajui." Kifungu hicho cha mwisho, neno hilo la mwisho, ndilo linalolifanya la kushangaza sana. Wanafikiri ya kwamba wamejazwa vizuri na Roho, wote wako tayari. Wakati wa Kanisa la Laodikia ni Wakati wa Kanisa la Kipentekoste, maana ni wakati wa mwisho wa kanisa. Luther alikuwa na ujumbe wake; Wesley alikuwa na ujumbe wake; na Wapentekoste walikuwa na ujumbe wao.

15 Pia, ulisema, "Kwamba kwa sababu una uvuguvugu, si moto wala baridi," misisimko ya kimwili, ujuzi wa Injili wa akili, "Kwa sababu" Yeye alisema, "uko jinsi hiyo, nitakutapika utoke katika kinywa Changu." Kwa maneno mengine, ilimfanya mgonjwa kuliona kanisa katika hali hiyo.

16 Na, kumbuka, walimtapika, na Yeye alikuwa nje ya kanisa akijaribu kuingia ndani tena katika Wakati ule mbaya sana wa Kanisa la Laodikia.

17 Mungu wa ulimwengu huu leo, mtu anayeabudiwa wa ulimwengu huu leo, ni Shetani. Nao watu hawajui kumwabudu Shetani, bali ni Shetani akijifanya kama kanisa, mnaona, kama kanisa. Wanamwabudu Shetani, wakidhani ya kwamba wanamwabudu Mungu kupitia kanisa, bali ni jinsi Shetani alivyofanya.

"Loo," unasema, "lakini ngoja kidogo; tunahubiri Neno."

Angalia nyuma hapa kwenye somo langu, usiku wa leo. Shetani alikuwa ndiye aliyemhubiri Hawa Neno, kwanza, "Mungu amesema," mnaona.

Ni kule kufasiri vibaya sehemu hiyo ya Maandiko inayotumika kwa siku hii. Yeye atawajulisha yote aliyofanya Yesu yalikuwa ni sawa kabisa. Yeye atawajulisha yote aliyofanya Musa yalikuwa ni mazuri kabisa. Lakini unapochukua ahadi ambazo Wao wamenena kwa ajili ya siku hii; basi Hizo zilihusika na wakati mwingine. Hilo tu ndilo tu analopaswa kufanya, mnaona, ni kuwafanya watu kuliamini hivyo, na hivyo—hivyo tu. Kwa kuwa, "Huwezi kuondoa Neno moja Kwake, wala kuongeza neno moja Kwake." Lakini hivyo ndivyo anavyofanya.

18 Watu, wakimwabudu Shetani bila kujua, wakidhani wanamwabudu Mungu; kama tunavyoonywa na unabii, katika Wathesalonike wa Pili. Hilo, hebu na tusome tu hilo, Wathesalonike wa Pili, mlango wa 2. Hebu na tulifahamu kidogo, nikiweza, mara moja. Ningetaka kusoma hayo. Ni ninii tu, ninaamini, Wathesalonike wa Pili. Nina Maandiko hapa. Katika Pili …

> *"Basi ndugu, tunakusihini, kwa habari ya kuja kwake Bwana wetu Yesu ... na kukusanyika kwetu mbele zake,"*

Sasa, mnaona, "kuja kwa Bwana, na kukusanyika Kwake," kama vile Mungu atakavyowakusanya watu Wake Kwake katika siku za mwisho. "Kukusanyika kwa watu mbele za Bwana, *Si mbele ya kanisa,* mbele za Bwana, kukusanyika pamoja mbele Zake."

> *8"Kwamba msifadhaishwe upesi hata . . . kuiacha nia yenu—wala msisitushwe, kwa roho, wala . . . neno, wala kwa waraka unaodhaniwa kuwa . . . ni wetu, kana kwamba siku ya Bwana imekwisha kuwapo.**
>
> *Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu, na yule mtu wa kuasi"* (mtu wa kuasi, angalia alivyo sasa) *"mtu wa kuasi afunuliwe, mwana wa uharibifu;"* (Huyo alikuwa Yuda, mnaona.)
>
> *"Yule mpingamizi ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu, ama kuabudiwa; hata Yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu."*

19 Huo udanganyifu wa kanisa la siku hizi! Mnaona, "mwana wa uharibifu," Ibilisi. "Mwana wa uharibifu," Ibilisi. Halafu, watu wakimwabudu Shetani katika siku hii, wakidhani wanamwabudu Mungu. Lakini wanamwabudu kupitia kanuni ya imani, madhehebu yaliyoundwa na mwanadamu na kanuni za imani zilizowafikisha watu kwenye udanganyifu ulio mkuu zaidi ambao ulimwengu hujawahi kuujua. Haidhuru kiasi gani Neno la Mungu lilivyoahidiwa kwa siku hii, linahubiriwa na kudhihirishwa, bado hawataliamini. Hawataliamini.

Basi kwa nini? Tunashangaa ni kwa nini. Kwa nini hali; kwa nini wasiliamini? Wakati Mungu aliposema angefanya kitu fulani, Naye anakitenda, na bado wao wanakiacha na kukikataa. Kama ambavyo Hawa alijua kwamba kile alichosema Mungu, Mungu angetenda; lakini alikipa kisogo, kusikiliza kile Shetani alichosema.

Kumbuka tu, katika nyakati zingine, daima imekuwa ni kitu kile kile. Katika kila wakati, imekuwa daima kwamba Shetani hujaribu kupotosha hilo Neno kwao, akiwafanya waone wakati mwingine.

20 Angalia, wakati Yesu alipokuja, mnaona, Shetani alikuwa katika kundi hilo la waalimu wa Kiyahudi, na marabi na makuhani, akijaribu kuwaambia washike sheria ya Musa, wakati Neno lenyewe lilisema ya kwamba katika siku hiyo Mwana wa Adamu angefunuliwa. mnaona, ya kwamba angejifunua Mwenyewe. Kwa hiyo walikuwa wakijaribu, mradi tu waliwaweka wa kidini, na kwa sheria ya Musa. Mnaona yale aliyofanya? Alikuwa akijaribu kuwaambia, "Sehemu hiyo ya Neno ni kweli kabisa, bali Mtu huyu si Mtu yule." Mnaona jinsi alivyo mdanganyifu? Hiyo ndiyo siku hiyo halisi ya udanganyifu.

21 Imekuwa, na sasa ni, Shetani akianzisha ufalme wake duniani. Hiyo ndiyo sababu hasa yeye anafanya jambo hilo, kwa kuwa anataka kuanzisha ufalme wake mwenyewe.

Kama mfanyi biashara ambaye si Mkristo, atafanya kila njama anazoweza kukufanya uone kitu kwa njia mbaya. Kama analo ku—ku kusudi fulani na faida ya binafsi katika kukufanya wewe utende hilo, kukufanya wewe ulione jinsi hiyo, atakuonyesha kila kitu anachoweza na kukuzuia uone ukweli wa mambo, kwa sababu anajipenda mwenyewe tu. Haidhuru kiasi gani anasema uongo na kudanganya, na lo lote zaidi, ana faida ya kibinafsi.

22 Na hiyo ndiyo sababu Shetani amefanya jambo hili. Naye ametenda kazi kupitia huduma kufanya jambo hilo, kama Mungu alivyoahidi angefanya. Sasa, yeye alianza kwa udanganyifu wa kidini katika Edeni, na ameendelea tangu wakati huo.

Si kwa kuanzisha kundi la wakomunisti. Wakomunisti hawana uhusiano wowote na jambo hili. Ni kanisa, hapo ndipo unapopaswa kuwa mwangalifu, mnaona. Si—si Wakomunisti ambao wangewapoteza walio Wateule. Kanisa ndilo litakalowapoteza walio Wateule, mnaona. Si wakomunisti; tunajua wanamkana Mungu, nao ni wapinga-Kristo, hakika wao, katika kanuni, bali wao si yule mpinga-Kristo. Mpinga Kristo ni wa kidini, wa kidini sana, naye anaweza kuyanukuu Maandiko, na kuyafanya yaonekane dhahiri sana.

Kama vile Shetani alivyofanya kule nyuma mwanzoni, alinukuu kila kitu moja kwa moja, "Mungu amesema, 'Usile kila mti wa bustani.'" Mnaona, alinukuu Hilo sawa sawa.

Yeye alisema, "Naam, tunaweza kula miti yote ya bustani, lakini kuna mti katikati ya bustani ambao Mungu alisema tusile, kwa kuwa, hata tusiuguse; maana, siku tutakayoula, siku hiyo tungekufa."

23 Akasema, "Loo, hakika hamtakufa. Lakini hebu niwape sababu ya Mungu kusema jambo hili, ni kwa sababu …" Mnaona, yeye sasa ni nini? Yeye alinukuu Ukweli huu, mnaona. Alisema, "Litawafungua macho yenu, na litawafanya mjue mema na mabaya. Mtakuwa kama Mungu basi, kama mnaweza kufanya hivyo."

Hilo ndilo tu analotaka kufanya, na hilo ndilo jambo lile lile analojaribu kufanya leo. Kumekuwa na udanganyifu wa kidini tangu mwanzoni kabisa katika Edeni, na umekuwa hivyo tangu wakati huo. Katika wakati wa Adamu, ilikuwa ni udanganyifu. Katika wakati wa Nuhu, ilikuwa ni udanganyifu. Katika wakati wa Yesu, ilikuwa vivyo hivyo. Na sasa ni vivyo hivyo, vivyo hivyo, udanganyifu wa kidini!

24 Sasa, tutaona dunia, wakati Mungu alipokuwa akiimiliki. Sasa, wakati Mungu alipokuwa ameitawala … aliiweka chini ya mamlaka Yake. Ndipo wakati Shetani alipoichukua, kwa kulikataa Neno la Mungu. Mungu wakati mmoja aliiweka dunia chini ya mamlaka Yake. Yeye aliiweka katika mzunguko wake. Aliiweka, akaifanya ifanye kazi. Yeye alifanya kila kitu, aliiweka katika miliki Yake. Sasa tutalinganisha hilo na baada ya Shetani kuitwaa na kuiweka kwenye miliki yake.

25 Sasa, ilimchukua Mungu miaka elfu sita. Haikumchukua muda mrefu namna hiyo, bali alichukua muda huo. Miaka elfu sita, kwa sababu tumefundishwa ya kwamba "siku moja Mbinguni ni miaka elfu moja duniani," na ilikuwa miaka elfu sita, ama siku sita ambazo Mungu aliiumba dunia. Sasa, ilimchukua Mungu miaka elfu sita kuifanyiza; akaipanda mbegu njema na kutoa kila kitu kwa jinsi yake. Kila kitu kinapaswa kazaa jinsi yake. Mbegu Zake zote zilikuwa njema, na kwa hiyo haina budi kuzaa kwa jinsi yake. Mungu alichukua miaka elfu sita.

26 Hatimaye, alipoitengeneza yote, na mwishowe .. mwishowe tukafikia makao Yake makuu, ya ulimwengu, katika mahali pazuri upande wa mashariki mwa Edeni, palipoitwa Bustani ya Edeni. Mungu aliyafanya makao makuu ya ulimwengu katika bustani ya Edeni, katika Misri, moja kwa moja upande wa mashariki wa bustani hiyo yalikuwa makao makuu.

27 Na juu ya hali yote, Yeye alimweka mwanawe na mke wa mwanawe, juu ya yote. Hiyo ni kweli. Hivyo

ndivyo Mungu alivyofanya. Aliwaweka katika mamlaka kamili. Wangenena na pepo, nazo zingeacha kuvuma. Wangenena na mti, nao ungesogea toka hapa hadi pale.

Simba na mbwa mwitu walilisha pamoja, na mwana-kondoo akalala pamoja nao. Hakukuwako na uovu wowote. Ilikuwa ni amani kamilifu, upatano mkamilifu, kila kitu katika ukamilifu, na wakati Mungu alipoiweka chini ya mamlaka Yake. Na angalia, Yeye alikuwa na ninii Yake … Alikuwa na ulimwengu Wake, Yeye alikuwa kila kitu kikifanya kazi. Alikuwa na kila kitu kikija. Kila kitu kinachokula mimea; hakuna kitu cha kufa, hakuna kitu cha kuharibiwa, hakuna kitu cha kuharibiwa. Kila kitu kikila mimea; hakuna cha kufa, hakuna cha kuharibika, hakuna cha kuharibiwa. Hakuna kitu … Ilikuwa ni kamilifu tu.

Na juu ya yote, Yeye aliwaweka watoto Wake wapendwa, mwanawe na binti Yake, mume na mke, kuitawala.

28 Mungu aliridhika sana! "Naye akapumzika toka kwa kazi Zake zote, katika siku ya saba," na kuitakasa sabato hii ya siku ya saba kwa ajili Yake.

Kwa sababu Mungu aliiangalia kila sehemu; baada ya kutumia miaka elfu sita akiifinyanga na kuitengeneza: akiifanya iwepo na akaweka milima na kufanya volkano; kuiinua milima na mambo yaliyotendeka, katika milipuko; akaikausha na akaitengeneza namna alivyotaka. Na ilikuwa mahali pazuri.

29 Hakukuwako na kitu kama hicho, zile paradiso kuu za Mungu! Na wale wanyama wakubwa wa kale na kadhalika, wakitambaa juu yake, na wale wanyama wakubwa; hawana dhara. Walikuwa wapole kama kitoto cha paka. Hawakuwa na cho chote hata; hakuna—hakuna maradhi, hakuna huzuni; hamna hata kijidudu kimoja cha maradhi juu ya dunia. Loo, ni mahali pa jinsi gani!

Wale ndege wakubwa wangeruka toka mti hata mti, na Adamu aliweza kuwaita kwa majina yao, nao wangerukia mabegani mwake na kumwimbia. Loo, mahali pa ajabu vipi alipokuwa napo Mungu!

30 Ndipo akafanya moja ya sifa Zake kutoka Mwilini Mwake. Mungu ana sifa katika Mwili Wake.

Kama vile, wewe ni sifa ya baba yako. Na, unaona, ulikuwa katika babu wa babu wa babu yako. Lakini katika hilo, tuseme, tutaichukulia kama kwamba ni wewe na baba yako. Sasa, hukujua chochote ulipokuwa ndani ya baba yako. Mbegu ya uhai hutoka kwa mwanamume. Mume ana chembe ya damu; mwanamke analo ya—yai; sasa, kwa hiyo, seli ya damu ina uhai ndani yake. Na, basi, wakati ulipokuwa ndani ya baba yako, kwa kweli hukuwa unajui kitu juu yake. Lakini, hata hivyo, sayansi na Neno la Mungu huthibitisha ya kwamba ulikuwa ndani ya baba yako, bali hukuwa na habari.

Lakini basi baba alitamani sana kukujua. Na kwa muungano wa kuunganika na mama, basi ukafahamika kwa baba. Sasa, wewe ni sifa ya baba yako. Unaonekana kama yeye, na una sehemu za mwili wako ambazo zinafanana na baba yako.

Sasa, hivyo ndivyo Mungu alivyokuwa hapo mwanzo. Kila mwana wa Mungu na kila binti wa Mungu alikuwa katika Mungu hapo mwanzo. Hukumbuki jambo hilo sasa, bali ulikuwa kule. Yeye alijua jambo hilo. Naye alikutaka uwe ili aweze kuwasiliana nawe, azungumze nawe na akupende, na kukupa mikono.

31 Hivi hutaki mvulana wako mwenyewe … Si ni siku kuu ambapo mvulana wako anaweza kuja nyumbani na kuketi mezani? Wakati anaporudi kutoka kwenye uwanja wa vita, ama cho chote kile, ana makovu; jinsi utakavyoandaa chakula cha jioni; unamchinja ndama aliyenona, ama cho chote kile, na kumtayarishia! Ni mwili na damu yako mwenyewe, naye alikuwa ndani yako. Hukumjua wakati huo, bali ulijua alikuwako.

32 Na kwa hiyo Mungu alijua ya kwamba tungekuwa hapa, lakini basi alituweka katika mwili ili tuweze kuwasiliana. Ili aweze kuwasiliana, Yeye alifanyika mmoja wetu wakati alipofanyika Yesu Kristo, Mwana wa Mungu Mwenyewe, utimilifu wa dhihirisho la Mungu. Kwa hiyo hilo lilikuwa ndilo kusudi la Mungu, kuonyesha sifa Zake katika ushirika.

Nilipokuwa katika baba yangu, sikujua kitu juu yake. Lakini wakati nilipokuwa mwanawe na kuzaliwa naye, nilikuwa ni sifa, sehemu ya baba yangu. Nawe ni sehemu ya baba yako.

Na kama watoto wa Mungu, sisi ni sehemu ya sifa ya Mungu iliyokuwa ndani Yake, iliyofanyika mwili kama Yeye alivyofanyika mwili, ili tuweze kuwa na ushirika mmoja kwa mwingine, kama jamaa ya Mungu duniani. Na hilo lilikuwa ndilo kusudi la Mungu hapo mwanzo. Naam, bwana. Hilo ndilo Mungu alilotaka hapo mwanzo.

Alikuwa amedhibiti kila kitu. Naye akamgeuza mwanadamu katika bustani ya Edeni, akiwa na uhuru wa kuchagua; useme, "Mwanangu, ni pako."

33 Ni mahali pazuri iliyoje! Mungu aliridhika sana, hata akarudi tu na kupumzika kutokana na kazi Zake zote. Kila mti haukutoa kamwe miiba na michongoma. Hakuna matunda yaliyoota katika mti wenye miiba. Kila kitu kilikuwa kikamilifu. Mbegu zote zilikuwa kamilifu. Kila kitu kilikuwa katika hali kamilifu.

Ndipo, hapo alipokwenda kustarehe kidogo, adui Yake akaingia kimya kimya kwa udanganyifu, naye akaitawala, kwa kufasiri vibaya mpango Wake kwa watoto Wake. Hapo alipoweka imani Yake katika mtoto Wake mwenyewe, kama uwekavyo tumaini katika binti yako wakati anapotembea usiku na mwanamume, unapomwamini mwanao wakati inapombidi kutembea na mvulana anayekunywa pombe au mvulana anayevuta sigara. Mnaona, Yeye alimtumaini mwanawe, ya kwamba asingefanya kosa lo lote, na angetimiza kila Neno alilosema. Lakini adui akaingia, kama yule mhuni mjanja ambaye angemchukua binti yako na kuwa na adabu mbaya; ama—ama mwanamke fulani angetoka, na mwanao, na kutenda kitu kile kile. Mnaona, aliingia kisiri. Adui wa Mungu aliingia kwa siri na kulifasiri Neno vibaya kwa Hawa.

34 Sasa, Yeye, kwa kuanguka huku, ameitwaa na kuimiliki Bustani ya Edeni, yeye mwenyewe. Aliitwaa. Na sasa, amekuwa na miaka elfu sita ya utawala wa udanganyifu; akidanganya watu, watoto wa Mungu, kama alivyotenda wakati huo. Kwa sababu, walikuwa wamewekwa kwenye uhuru wa kutenda walilolitaka. Na kuamini kwamba wangetenda lililo sahihi, ama kutumaini wangetenda lililo sahihi, basi wakaja na tendo lisilo sawa, na wakauza haki yao ya mzaliwa wa kwanza, kama alivyofanya Esau, kwa ajili ya ulimwengu. Na Shetani alishinda, na akaichukua. Naye amekuwa na miaka elfu sita ya kujenga Edeni yake, kama vile Mungu alivyokuwa na miaka elfu sita kuimaliza Edeni Yake. Na kwa udanganyifu, udanganyifu wa Neno au wa watu, sasa, aliweka Edeni yake mwenyewe humu duniani katika dhambi.

35 Edeni ya Mungu ilianzishwa katika haki. Edeni ya Shetani imeanzishwa katika dhambi, kwa sababu Shetani ni dhambi. Mungu ni haki, na ufalme wa Mungu ulianzishwa katika haki, na amani, na Uzima. Na uanzishwaji wa Shetani uko katika dhambi, na dhambi ya kidini.

Angalia jinsi alivyodanganya, udanganyifu wake, kama alivyosema angefanya. Yeye aliahidi kufanya jambo hili. Kuna mtu aliyejua jambo hilo? Hebu na tufungue Isaya, kama unataka baadhi ya Maandiko haya. Kama wewe … Ninapaswa kunukuu zaidi ya hayo, nadhani. Hebu na tufungue Isaya sura ya 14, kwa muda kidogo tu, na tuone yale Shetani aliyosema hapa, kwa muda kidogo tu. Katika Isaya 14, tutalisoma, na tuone yale jamaa huyu amefanya. Isaya 14, kuanzia na kifungu cha 12.

> *Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa!*
>
> *Kwa kuwa ulisema moyoni mwako, Nitapaa juu mbinguni, nitakiinua kiti changu juu ya nyota (hao ni wana), nyota za Mungu; nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, … upande wa kaskazini;*
>
> *Nitapaa kupita vimo vya mawingu; nitafanana na yeye Aliye juu.*

36 Sasa linganisha hilo hapa na yale Maandiko mengine katika Wathesalonike, muda uliopita, jinsi alivyosema, "Anaketi katika hekalu la Mungu, akijiinua mwenyewe juu ya kila kiitwacho Mungu, ili kwamba yeye kama Mungu, anaabudiwa kama Mungu duniani."

Huyo hapo mungu wa ulimwengu huu niliyemwahubiria kuhusu Jumapili iliyopita. Huyu hapa leo katika udanganyifu, ile saa danganyifu, wakati huo mkuu sana tunaoishi. Ni wakati wa fahari sana wa nyakati zote, kwa sababu tunaukabili ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu tena; tunakabiliana na Edeni tena. Lakini papa hapa kwenye wakati huu, kila udanganyifu na kila ujanja ambao aliwahi kuutumia na ameweza kudanganyia, ameukusanya wote pamoja na kujiimarisha, na kushuka kama Mungu, na kujiweka mwenyewe mahali pa Mungu, wa kidini, naye anaweza kunukuu Maandiko naye anaweza kukuambia Maandiko, kama vile Shetani alivyofanya kwa Hawa katika Bustani ya Edeni. Lakini kuacha sehemu moja ya hilo ndilo lote limpasalo kutenda, kufanya pengo hilo, ambapo sumu ya fundisho la Shetani inaweza kuingilia, kama chujio la mtu mwenye busara ambalo tulikuwa tukizungumzia usiku ule mwingine.

37 Sasa, yeye alisema angejiinua juu ya Aliye Juu sana; angepanda juu ya mawingu na nyota, naye angeketi pale kama Mungu, na kuwa juu ya Aliye Juu sana. Naye amefanikiwa kutekeleza vitisho vyake. Hakika amefanikiwa sana katika kutekeleza vitisho vyake, kwa watu kumruhusu kuelezea, katika kila wakati, thamani ya Neno la Mungu lililoahidiwa kwa wakati huo. Hivyo ndivyo hasa alivyofanya. Katika kila wakati, alilielezea.

38 Katika siku za Nuhu, alieleza ya kwamba haingewezekana kunyesha kutoka mbinguni, kwa kuwa, "hakuna mvua huko juu." Injili yake kuu ya kisayansi aliyohubiri katika bustani ya Edeni! Yeye angeweza kupeleka vyombo kwenye mwezi, na kudhibitisha hakuna unyevu huko. Lakini Mungu alisema mvua itakuja. Lakini Shetani alifanikiwa, na akatia sumu akili za watu, kwa utafiti wa kisayansi, ya kwamba, "isingewezekana." Lakini ilitendeka. Mungu alisema ingetendeka, na ilitendeka. Alifanya hivyo.

39 Sasa, katika siku za—za Yesu, alifanya jambo lile lile. Alitia sumu akili zao tena kwa udanganyifu, mnaona, akilifasiri Neno vibaya. "Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, sasa hebu nikuone ukifanya jambo fulani kuhusu hilo."

Yesu hakujipumbaza kwake. Kamwe hakufanya hivyo. Mungu hajipumbazi. Halazimiki kujibu chochote ambacho Shetani anauliza. Yeye alikuwa tu … Yesu alisema, "Imeandikwa, 'Usiishi … Mtu hataishi kwa

mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.'" Mnaona, Yeye haikumlazimu kujipumbaza kwake. Haikumlazimu kutengeneza mkate. Angeweza kufanya hivyo, bali angekuwa akimsikiliza ibilisi, kwa hiyo hakulazimika kumsikiliza ibilisi.

40 Na tena ni dhambi ya kidini, kama hapo mwanzo, ni ya udanganyifu sana. Liangalie sasa. Si tu dhambi ya kale ya kila siku,kuzini na kulewa, na kutumia Jina la Mungu bure. Si hivyo. La.

Mnakumbuka miaka mingi iliyopita, wengi wenu hapa, washiriki wa siku nyingi, mnakumbuka yale mahubiri niliyohubiri juu ya *Kuadhirika Hukumuni*. Yule kahaba, hatafadhaika pale. Anajua anakwenda wapi. Mlevi hataadhirika kule. Mfanya magendo ya pombe, mcheza kamari, mwongo, mwizi, yeye hataadhirika. Lakini, mtu huyo anayefikiri yeye yuko sahihi, hapo ndipo kuadhirika.

Huyo ndiye yule mtu, aliyekuja akasema, "Bwana, sikuhubiri Injili; sikutoa pepo katika Jina Lako?"

41 Yesu alisema, "Ondokeni kwenu … toka Kwangu, ninyi mtendao maovu. Hata sikujua." Hapo ndipo penye kuadhirika, mnaona, huo udanganyifu.

Hilo ndilo ambalo wakati wote . . . hapo ndipo ambapo sieleweki sana. Si kwamba nataka kuwa tofauti. Sitaki kuwa tofauti, bali sina budi kuwa mwaminifu. Nina Ujumbe, na Huo hauna budi kuwaendea watu. Hilo huufanya usieleweke sana miongoni mwa watu. Wanafikiri ninampinga kila mtu. Kama wangejua tu, nampenda kila mtu, ninajaribu niwezavyo kuwaletea iliyo Kweli, kama inavyowekwa moyoni mwangu, na jinsi inavyowekwa katika Biblia, hapa. Na Mungu anathibitisha hilo kuwa Ukweli, kwa hivyo hakuna kitu kingine cha kufanya kulihusu. Ama wanaliangalia au hawaliangalii.

42 Mnaona, hawataki kuliona, kwa sababu wamekwisha uza tayari, wameuza haki yao ya mzaliwa wa kwanza kwa taratibu fulani, dhehebu fulani, kujaribu kwa haki yao ya mzaliwa wa kwanza kufika Mbinguni juu ya msingi wa taratibu ya dini, ambayo Shetani ndiye kichwa cha kila sehemu yake. Mungu hajawahi kuwa na dini ya kidhehebu, kwamwe hajawa nayo. Nao wanajiuza kwa hilo, ambapo wao, kundi la watu, wanalifasiri Neno na kusema linamaanisha *hili* na linamaanisha *lile*.

Mungu hahitaji mfasiri. Yeye hujifasiria Mwenyewe. Yeye hahitaji mtu mwingine yeyote kumwambia jinsi ya kufanya jambo hilo. Yeye ni mwenye mamlaka. Yeye alisema jinsi atakavyofanya jambo hilo, na hivyo ndivyo anavyopaswa kulitimiza Neno Lake. Wakati aliposema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," Yeye alimaanisha hilo tu. Lo lote alilosema lingetukia, Yeye alisema lingetukia katika siku hizi za mwisho, ya kwamba Yeye angefanya mambo fulani, Naye alifanya. Halazimiki kumuuliza ye yote kama kuna muda au la. Yeye anajua wakati ni nini, na mpango ni nini.

43 Sasa, Shetani, huyu mdanganyifu, kama ilivyonenwa katika Mathayo 24:24 na udanganyifu mwingi mno. Sasa, tunaona kwamba kwa mpango wake wa injili ya ujuzi: elimu bora, elimu ya maadili ya hali ya juu, ustaarabu, na kadhalika, imewaloga watu ambao wanataka kumtumikia Mungu katika kuamini uongo wake.

Hawa hakutaka kufanya jambo hilo, bali alimwonyesha jinsi ilivyokuwa hekima zaidi ndani yake. Hakujua; alitaka kujua. Yeye hakufahamu, bali alitaka kuelewa. Naye Mungu akamwambia asijaribu kuelewa.

Ninawezaje kufahamu lolote la mambo haya? Siwezi kuyafahamu. Ninayaamini. Si lazima niyafahamu. Mungu ni imani, wala si ufahamu. Tunaamini tu yale aliyosema.

44 Sasa, linganisha Edeni ya Mungu na ya Shetani sasa, baada ya miaka elfu sita ya kupotosha tafsiri ya kweli ya Neno la Mungu lililoahidiwa na wakati. Hebu na tulilinganishe sasa, na tuone mahali tunapofikia. Kama vile alivyofanya kwa kanisa katika—katika wakati wa Kristo, katika Yesu, akijaribu kuwazuia—kuwazuia wana waaminifu wa Mungu wasijue Kweli. Hilo ni la Mungu. Mungu aliwaweka wanawe hapa, sifa Zake, kushiriki pamoja Naye kwa kulisikia Neno Lake.

45 Vipi kama baba yako angekuambia…nawe u mwana mwaminifu kwa baba yako, naye alikuambia, "Mwanangu, usiende kwenye maji yale kule, kuogelea, kwa sababu kuna mamba katika maji yale," na mtu arudi na kusema, "Hakika, maji mazuri kama hayo, hayana mamba."? Sasa utamsikiliza nani? Kama wewe ni mwana halisi, utamsikiliza baba yako.

Na mwana ama binti halisi wa Mungu huchukua Neno la Mungu kwanza. Sijali mtu mwingine yeyote anasema nini juu yake, wanalichukua Neno la Mungu kwanza. "Kuna sumu katika kikombe," nao huamini hilo.

Kuwa na imani katika Neno Lake lote, Mbegu Yake, kulileta Edeni ya utakatifu, upendo, na Uzima wa Milele. Hilo ndilo ambalo Edeni ya Mungu inatoa, utakatifu. Nayo ilileta Edeni ya utakatifu, upendo, ufahamu, ukamilifu, na Uzima wa Milele. Hivyo ndivyo Mungu anavyopanda, Neno Lake, Uzao Wake. Hivyo ndivyo Kanisa Lake litakavyokuwa mwishoni; Itakuwa ni jambo lile lile.

46 Angalia, hili hapa wazo. Usisahau jambo hilo. Nitaufikia wakati mwingine ama Ujumbe mwingine.

Lakini, mnajua, Mungu alisema, "Kila mbegu na izae kwa jinsi yake." Hiyo ni amri ya Mungu? Sasa mhubiri yeyote ana faida gani, ama mtu mwingine yeyote, kujaribu kulifanya Neno hilo kusema jambo lingine? Mnaona, kila Neno la Mungu ni Mbegu. Yesu alisema hivyo, "mbegu aliyoipanda mpanzi." Kwa hiyo kama Marko 16 ni Neno la Mungu, litazaa kwa jinsi yake. Kama Malaki 4 ni Neno la Mungu, litazaa kwa jinsi yake. Na kila ahadi nyingine haina budi kuzaa kwa jinsi yake.

47 Mnaona, unamuona Shetani hapa katika kujibadilisha? Yeye anajaribu kusema, "Siyo, hivyo." Mnaelewa jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mnaona, Shetani asema, "Loo, Hilo si la siku hizi. Hilo, hilo—hilo ni … Hilo lilikuwa ni la wakati mwingine. Hilo, hilo hata halimaanishi hilo."

Kila mbegu lazima izae kwa jinsi yake! Hivyo ndivyo ambavyo Mungu aliimarisha Edeni yake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Na ndilo hili hapa, hivyo ndivyo ambavyo Mungu huliimarisha Kanisa Lake, kila Neno kwa jinsi yake. "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Mnaona? Shetani, atachukua kitu kingine. Lakini Mungu alisema, "Kila mbegu kwa jinsi yake."

Kama ahadi ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

Sasa kanisa linasema, "Jiunge na kanisa. Kariri kanuni za imani. Ijua katekisimo." Hakuna mambo kama hayo katika Biblia nzima.

Lakini, Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: katika Jina Langu, watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; kama wakishika nyoka, au wakinywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Ni mtu gani atakana hilo? Mnaona?

48 "Kila mbegu itazaa kwa jinsi yake." Kama wewe ni mbegu ya Mungu, sifa, mwana wa Mungu, basi Neno la Mungu linapandwa ndani yako. Mnaona? Na ndipo unapolisikia Neno la Mungu, "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu; mgeni hawatamfuata." Mnalipata? "Ndipo kila mbegu hutoka kwa jinsi yake."

49 Sasa tunaona, kwamba kila mbegu ikizaa kwa jinsi yake, hakukuwa na mauti katika ile mpya … katika ile Edeni. Hakutakuwa na mauti katika Edeni mpya. Mnaona, hakukuwako na, kitu kingine ila utakatifu, usafi, na Uzima wa Milele.

Sasa, kwa kutokuamini katika Neno lote la Mungu kumeleta mbegu ya uchafu katika Edeni ya Shetani. Sasa tunaingia ndani ambapo Shetani amechukua kiti cha enzi kama mpinga Kristo, kati—katika Edeni ya dunia hii, Edeni ya dhambi, dini iliyopotoshwa. Alianza si katika, "Mimi ni Shetani. Mimi ni yule malaika mkuu." La, si juu ya jambo hilo, bali juu ya kupotosha Neno la Mungu. Na hivyo ndivyo alivyouleta ufalme wake, katika kila wakati. Na sasa katika wakati huu mkuu wa udanganyifu, tayari kuchukua kiti chake cha enzi, kwa watu wake! Amejijengea Edeni ya kiakili, ya elimu, ya kisayansi, sawa, wahubiri wa kisayansi, kanisa la kisayansi, theologia ya kisayansi, kila kitu ni cha kisayansi. Kila kitu kiko juu ya msingi wa maarifa. Kanisa lote limejengwa juu ya maarifa. Haijajengwa juu ya imani.

50 Wakati mmoja nilienda kufanya mkutano kwa kanisa la mtu fulani. Ilikuwa ni ukumbi mkubwa wa magharibi. Mtu mzuri, naye alikataa mambo haya tunayozungumzia. Lakini hata hivyo, yeye alikuwa … Nilimpenda; mtu mzuri, mzee. Wakati kusanyiko lake lilipotoka … Liliketi karibu watu elfu sita. Wakati kusanyiko lake lilipotoka, katika ibada ya alasiri, yapata elfu moja mia tano, wote walikuwa wasomi waliovalia nadhifu. Niliketi pale na kuwaangalia.

Alihubiri mahubiri mazuri sana, mtu huyo alihubiri. Na halafu aliuliza kama ye yote alitaka kumkubali Kristo; wainue tu mikono yao. Wala hakuna mtu aliyeinua mikono yao. Na hatimaye mwanamke mmoja akainua mikono yake. Akasema, "Vema, sasa u Mkristo," na akamweka kwa ubatizo. Na kisha alipotoka ... Yeye aliweka wakfu mtoto mchanga, akambusu mtoto huyo mchanga na kufanya maombi juu yake, na akatawanyisha kusanyiko.

51 Wakati kusanyiko lake lilipotoka; watu wote wazuri, wasomi, wenye elimu. Ndipo nilikuwa nimesimama kando, kumpa mkono mtu huyo na kumtakia mafanikio kwa Mungu, alipokuwa akitoka.

Na nilipofanya hivyo, kundi langu lilikuja. Wasingeweza kuwaruhusu kuingia wakati umati wake ulipokuwa pale. Hapa laja langu katika magari ya kusukumia wagonjwa, machela, makoti ya wakichaa, wenda wazimu na kadhalika. Mnaona tofauti? Hivyo ndivyo ilivyo. Hilo ndilo jambo ninalonena habari zake, mnaona. Mnaona, ni kitu tofauti.

52 Ambapo, kwa ujuzi wa kisayansi, unaweza kufanya injili ya kueleweka, ya kwamba, wewe, "Yeye amwaminiye Yesu Kristo hatahukumiwa," mnaona

Lakini, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," mnaona, yeye anashindwa kuliweka Hilo mle ndani, mnaona. Alimwamini Yesu Kristo, ameokoka, kama ishara hizi zinamfuata mwamini.

"Na yeye alisikiaye Neno Langu," si kujifanya kitu fulani, si kulisikia na masikio pekee, lakini, "kulielewa." Mtu yeyote anaweza kuisikia; kahaba anaweza kuisikia na kuendelea kuwa kahaba; mnaona,

mlevi anaweza kusikia Hilo; mwongo anaweza kuisikia na bado adumu mwongo. Lakini, "Yeye afahamuye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele." Haya basi, mnaona.

Na hakuna mtu anayeweza kufanya jambo hilo isipokuwa Mungu amemchagua tangu zamani. Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Amina. Yote ni mamlaka na kujua tangu zamani kwa Mungu. Yeye anaishi peke yake na hakuna mtu anayemwambia la kufanya.

53 Sasa, kwa kutoamini, na kuchukua Neno lote la Mungu, kumeleta mbegu ya kutoamini, uchafu, ya dhambi, chuki, na kifo cha milele kiko katika wakati huu wa dhambi, wa kanisa la kiakili. Sasa mmelipata? Katika siku hii, ambapo ulimwengu mzima ni wa kidini! Je! Ulijua jambo hilo? Ulimwengu mzima ni wa kidini. Na katika wakati huu wa kidini, makanisa makubwa kila kona; kila kitu, kitu hicho chote kinaishia kwa Shetani kuabudiwa. Hili hapa, papa hapa katika Biblia. Hiyo ni kweli. Na katika seminari hizi za kielimu, za kitheolojia ambazo zimemleta mtu mwenye elimu ambaye amefunzwa jinsi ya kunena, la kufanya, jinsi ya kutengeneza mihemko yao; na kila kitu kama saikolojia, miaka mitatu na minne, kujua jinsi ya kushughulika na akili za mtu. Mnaona, ni …

Roho wa Mungu si kitu ambacho, wewe, kimefundishwa ndani yako. Ni kitu ambacho kimekusudiwa tangu zamani ndani yako, kwa mkono wa Mwenyezi Mungu. Juzi wako hauwezi kuelimishiwa ama kufunzwa ndani yako Umechaguliwa tangu asili, kwa mkono wa Mungu na kujua tangu zamani kwa Mungu, ndani yako. Hiyo ni kweli.

54 Sasa, alileta Edeni hii kubwa ambayo sasa wanaishi ndani yake, Edeni ya kanisa la ulimwengu. Wote wanaunganika pamoja sasa kwenye Halmashauri kuu ya Ekumeni, nao watakuwa na kanisa la ulimwengu wote wakija chini ya kiongozi mmoja, ambapo Shetani atatawazwa, kweli kabisa.

Na mwito wa mwisho unatoka kumshika Bibi-arusi kabla hajaingia katika hiyo. Kwani mara aingiapo katika hiyo, yeye amechukua alama ya mnyama, na amehukumiwa, hatatoka kwake kamwe. Hiyo ndiyo sababu, kusema, "Tokeni kati yao, enyi watu Wangu," kabla halijaingia ndani yake, mnaona. "Tokeni kati yao, mkatengwe nao."

55 Sasa, chuki na mauti, na utengano wa Milele na Mungu, katika Edeni hii; tamaa mbaya, uchafu, upotovu, (vipi?) kwa kupanda mbegu mbaya.

Inanikumbusha juu ya ono nililoona kabla sijawahi kukutana na Wapentekoste, ya Mtu huyo akizunguka ulimwenguni, katika mavazi meupe. Mmenisikia nikilisimulia mara nyingi. Na mmoja akaja nyuma Yake, akipanda mbegu za mifarakano.

Lakini aliishinda kwa haki, katika Hawa … katika bustani ya Edeni, kwa tamaa ya Hawa kwa ajili ya dhambi; tamaa ya Hawa, ya dhambi. Halafu, kama Hawa alitamani maarifa, ilikuwa ni dhambi.

Na wakati tunapotamani maarifa, tunataka Ph.D., LL.D., ni dhambi kufanya hivyo. Huo ni msemo mzito, lakini hiyo ni Ukweli. Haidhuru ni mzito kiasi gani, bado ni Ukweli, mnaona. Kutamani maarifa, ufahamu!

Jambo ni kwamba, ni, leo hatujaribu kuliweka Neno la Mungu katika mioyo ya watu. Tunajaribu kujiimarisha. Makanisa yanajaribu kuanzisha fundisho la kanisa, katika moyo wa mtu.

Tumeamriwa kuliimarisha Neno la Mungu. Paulo alisema, "Sikuwajia kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, lakini naja kwenu kwa nguvu; katika madhihirisho ya Roho Mtakatifu ili imani yenu ikae katika Mungu." Haya basi.

56 Mwanadamu hapaswi kujiimarisha. Tunaliona miongoni mwa … Hebu Mungu na atende kitu kwa mtu na amtume, utaona kila mtu akijaribu kumuigiza. naona, wanajaribu kujiimarisha wenyewe. Kila mtu, "Nilifanya jambo hili. Mimi, mimi, langu, dhehebu langu, mimi, hili," wakijiimarisha wenyewe. Tunahubiri nini, sisi wenyewe ama Ufalme wa Mungu?

Thibitisha Neno la Mungu. Ondoa kutokuamini na kuuweka Ufalme wa Mungu katika moyo wa mwanadamu. Wala Ufalme wa Mungu hauwezi kuanzishwa katika moyo wa mtu isipokuwa Mungu amemfanya mtu hivyo. Hawezi kuwekwa katika…

Na, kumbukeni, sehemu ya udanganyifu, ambayo watu wanafikiri ya kwamba ni kweli. Mnaona. "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu." Kila mwenye akili anaonekana ni sahihi.

57 Kama nilivyowaambia Jumapili chache zilizopita; niliposimama karibu na mtoto wangu mchanga aliyekuwa anakufa, na Shetani akisimama hapo na akasema, "Baba yako yuko pale, alifia mikononi mwako usiku uliopita. Huyo hapo mkeo amelala pale kwenye—katika chumba cha maiti, na huyu hapa mtoto wako anaenda. Na unamwomba akujibu, na ameshusha nini yako ... kivuli juu yako. Sasa, na hata hivyo Yeye ni Mungu mwema, na hata hivyo ulisema alikuwa Mponyaji. Nawe, ambaye unasimamia kile ulichosema ni sawa, umekosea." Loo, kila sababu, kila akili ilibidi ikubaliane kwamba ilikuwa ni kweli; naye

alikuwa sahihi, kiasi hicho.

Hivyo ndivyo alivyokuwa sahihi wakati alipomwambia Hawa, "Macho yako yatafunguliwa, nawe utajua mema na mabaya. Nanyi mtakuwa kama miungu, kwa njia hiyo, mkijua mema na mabaya," kwa sababu Mungu hakuwaruhusu kujiona wenyewe bado, ya kwamba walikuwa uchi. Kwa hiyo walijua wangejua mema na mabaya; Naye alikuwa sahihi. Lakini, mnaona, ilikuwa ni kinyume cha Neno la Mungu.

58 Vivyo hivyo wahudumu katika seminari, wakijifunza theologia za mwanadamu; yaweza ionekane sawa, yaweza iwe ufahamu mzuri ya jambo hilo, lakini ni makosa!

Haitupasi kulielewa. Tunaliamini kwa sababu Mungu alisema ndivyo lilivyo, na hilo latosha milele. Jambo lote, hiyo ndiyo njia ya kuliamini.

Loo, jinsi Hawa alivyotamani kuwa na Ph.D., mnaona, jinsi alivyotamani kuwa mwerevu kuliko alivyokuwa!

59 Angalia jinsi wanavyofanana, mwanamume na mkewe … Sasa angalia, mwanamume na mke, wote wawili wakiwa uchi katika bustani ya Edeni, Edeni ya Mungu.

Sasa nitafunga. Nilisema nitashikilia kwa dakika chache tu. Angalia, angalia sasa, tunapofunga.

Linganisha jambo hili sasa, ni sawa jinsi gani na huyo mtu na mkewe, wote wawili katika Edeni ya Mungu, bila nguo moja, wala hawakujua. Kwa maana kwa nini hawakujua jambo hilo? Kwa kuwa walikuwa wamefumbwa hisi zao za kujijua wako uchi kwa Utaji Mtakatifu wa Roho Mtakatifu. Wangeweza kutazamana moja kwa moja, wala hawakujua ya kwamba walikuwa uchi. Walikuwa wamefunikwa na Roho Mtakatifu, wa utakatifu. Walikuwa wametiwa utaji.

60 Utaji wa Mungu, hata leo, unaweza kuangalia na usitamani. Wanageuza vichwa vyao. Ni Pazia Takatifu, mnaona, Pazia Takatifu. Mungu alikuwa na macho yao … wote wawili, mmoja alikuwa mwanamume na mwingine alikuwa mwanamke, nao hawakujua walikuwa uchi, kwa sababu utakatifu wa Mungu uliyaficha macho yao. Angalia, Mungu alificha dhamiri zao dhidi ya dhambi, kwa Pazia Takatifu.

Laiti tungalikuwa na wakati wa kuweka juu ya jambo hilo, dakika chache. Angalia hapa, "Kwa maana yeye, mwabudu akisha kusafishwa mara moja," Waebrania, "mwabudu akisha kusafishwa mara moja, asingejiona tena kuwa na dhambi." Dhambi imempita.

61 Nilimsikia Ndugu Neville akisema, asubuhi ya leo; huenda mtu fulani alikuwa akimwuliza kwa nini sikuhubiri juu ya Roho Mtakatifu, kwa nini sikufanya jambo *hili*. Hili hapa. Roho Mtakatifu ndiye tendo ndani yako. Ni Uzima, si mhemko; si ushuhuda wa kimwili. Bali ni Mtu, Yesu Kristo, Neno la Mungu lililoimarishwa moyoni mwako, kulihuisha kila Neno la wakati huu. Sawa. Mwangalie Roho Mtakatifu akitenda kazi, si katika maonyesho sana; bali, katika matendo, kile anachofanya kulingana na Neno.

62 Angalia sasa Roho Mtakatifu, wa Neno Takatifu la Mungu, alikuwa na mwanamume na mwanamke uchi, wala hawakujua. Jinsi lilivyo zuri, Uzima wa Neno; ile Mbegu, Neno!

Mungu alisema, "Kuna mti katikati ya bustani, mwanamke. Na katikati ya bustani kuna mti huu; hata msiuguse. Kwa maana, siku utakayokula, siku hiyo utakufa." Walikuwa wametiwa utaji mtakatifu, hawakujua kitu juu yake, hawakuthubutu kuugusa.

Walikuwa wametiwa "utaji mtakatifu." Walikuwa salama katika hema kubwa ya Mungu. Walikuwa hai. Hawakuwa na mauti karibu nao. Haleluya! Walikuwa na upendo mkamilifu mmoja kwa mwingine, Uzima mkamilifu milele. Walikuwa na upendo mkamilifu, ufahamu mkamilifu wa upendo wa Mungu. Walikuwa na Neno la Mungu, na walilitimiza. Nao walikuwa hai na salama katika Edeni ya Mungu, bila mauti, hata kidogo, kote.

63 Ndipo, Shetani akamfanya Hawa asikilize injili yake ya theolojia, injili ya maarifa, elimu ya juu, maadili ya juu, ustaarabu bora, elimu ya juu, na kadhalika; basi wakati alipomfanya ninii … mwanamke asimame na kumsikiliza kwa dakika moja, kwa hoja zake (ambazo tumeamriwa kuzitupa chini), wakati alipomfanya azisikilize.

"Sasa, angalia hapa, kanisa ni *fulani*. Limeanzishwa kwa muda mrefu sana. Sisi ni moja ya makanisa ya kale sana nchini. Meya wa mji huenda." Sijali ni kitu gani, mnaona. Kama ni kinyume cha Neno la Mungu, lipinge. Huyo ni adui wako. Cho chote kinachopinga Neno ni adui yako.

Kila kitu kilicho kwa Neno ni ndugu yako. Yeye ni sehemu yako.

64 Angalia, aliondoa ule Utaji Mtakatifu, ili aone jinsi kujuana kimwili kulivyo hasa; linganisha hilo, jinsi tamaa mbaya ingefanya. Aliondoa ule utaji machoni pake, kile kitu kitakatifu ambacho Mungu alikuwa ameweka machoni pake. Alitaka maarifa, ajue ilivyokuwa, kwa hiyo aliondoa ule utaji apate kuona ilikuwa nini. Yeye alimsikiliza Ibilisi, na angalia ni mahali gani lilimweka.

Wametenda jambo lile lile katika kila wakati baadaye, siku zote wakienda upande wa akili; na sasa wamejenga ufalme wa Shetani, maarifa, mbegu yake aliyopanda, nayo imeufanya ulimwengu kuwa Edeni ya kifo.

65 Sasa angalia. Sasa angalia Ufunuo 3, Wakati wa Kanisa la Laodikia. Unawaza hayo niani mwako.

Sasa angalia. Yeye, Hawa, ni malkia wa Shetani. Mnaona, Shetani, yule nyoka, alimfikia Hawa kabla Adamu hajampata. Mnaona? Hiyo ni kweli. Kwa hiyo akamdanganya, mnaona; kwa hiyo Shetani, yule nyoka, alikuwa ni mume wa Hawa kabla Adamu hajajua. Mnaona, alimdanganya. Biblia ilisema alifanya hivyo, naye alijua alikuwa uchi, basi. Mnaona?

66 Sasa angalia Wa—Wakati wa Kanisa la Laodikia. Yeye, Hawa, ameketi kama malkia wa Shetani. "Yeye ni tajiri katika mali ya kilimwengu; kipofu, uchi tena, wala hawajui," kama tu ilivyokuwa katika Edeni ya Mungu. Lakini sasa, si kwa sababu Pazia Takatifu liko juu ya uso wake, bali uji wa tamaa mbaya. Kwamba, yeye alivua Utaji Mtakatifu wa Mungu, na kuvaa utaji wa maarifa, kwa ajili ya tamaa mbaya. Na sasa ana utaji wa tamaa mbaya, hata yu "kipofu" kwa jambo hilo kuwa ni dhambi. Yeye ni "uchi" barabarani, "wala hajui." Yeye ni kahaba mtaani. Wanawake waliovaa hizi kaptura, machoni pa Mungu, ni kahaba, "wala hawajui."

67 Angalia, wachukue wanawake wetu. Sasa, kama unataka kuona kanisa liko katika hali gani, angalia jinsi wanawake wanavyotenda. Yeye daima huwakilisha kanisa. Katika Edeni ya Shetani, ya dhambi na kutokuamini, upotovu wa kidini; ufalme uliopotoshwa. Badala ya kuchukua Neno la Mungu, wamechukua elimu ya kiakili ya mwanadamu. Na badala ya kulichukua Kanisa, walichukua dhehebu, nao wanalileta kwa kiongozi mmoja mkuu.

68 Sasa angalia, wamepotoshwa kutokana na kutokuwa na hatia. Usikose jambo hili sasa. Kanisa limevaa utaji huu wa tamaa mbaya. Angalia kile limemtendea. Li—limepotoshwa kutoka kutokuwa na hatia hata maarifa. Mnaona? Ule Utaji Mtakatifu, hakuwa na hatia; akiwa na ule utaji wa tamaa mbaya, yeye ni maarifa. Anajua ni wa kupendenza. Anajua kile unachofanya, waona. Ni tunda, mti wa kutamaniwa, ukimfanya mtu kuwa na hekima. Mnaona? Yeye amepotoshwa kutoka asiye na hatia hata kufikia maarifa, kutoka utakatifu hadi uchafu na tamaa mbaya, na kutoka Uzima hata mauti.

Ufalme huu hauna budi kufa. Ufalme huu utakufa! Mungu wa Mbinguni atauangamiza usoni pa dunia.

69 Angalia, katika upotovu huu, imekuwa kutoka kwa mwanamume hadi mwanamke, na kutoka kwa mwanamke hadi kwa mwanamume, "wala hawajui." Tunda zuri sana la Edeni ya Shetani kama utatazama barabarani leo hii, uwaangalie watu wetu wa kisasa.

70 Angalia, ilikuwa Hawa ambaye Shetani alitumia kumfanya Adamu atende dhambi kwa nguvu zake za tamaa mbaya. Sasa vivyo hivyo, tukifanya jambo lile lile leo. Angalia, nywele zilizokatwa, nyuso zilizopodolewa, nguo za kutamanisha, mnaona, yeye hutenda hilo, na hajui kwamba kila moja ya mambo hayo ni kinyume cha Neno la Mungu! Kukata nywele zake, kumfanya mwanamke asiye na heshima, kahaba. Kuvaa kaptura, humtia aibu. Kuvaa mavazi ya kutamanisha, humfanya kahaba. "Naye hajui jambo hilo," si kwa sababu ya utakatifu wa Mungu; kwa sababu ya tamaa ya Shetani. Alimfanya … Yeye humfanya Adamu wake kumtamani.

71 Alivua nguo ambazo Mungu alimvisha, huko nyuma Edeni, kwa ajili ya safari yake kupitia—kwenye jangwa hili. Alizivua. Alijivua nguo. Wakati, Mungu alikuwa amemfunika kila mahali kwa ngozi; ameanza kukata nywele zake kidogo-kidogo kila wakati, sasa, amerudi ambapo alikuwa hapo mwanzo

Sasa yeye amemfanya Adamu wake avae nguo zake za ndani. Mwanamume, akivaa hizo kaptura, zinazofanana na za kike, na kutoka nje huku, sidhani kuna uanaume wa kutosha kwake. Ndiye jike kuu sana ninalojua. Mnaona? Mnaona, yeye amemfanya Adamu wake aliyepotoka kutenda kama yeye, mnaona, amevaa nguo zake za ndani. Aliona yale angeweza kufanya huko ng'ambo wakati alipovua nguo zake zote ila zile za ndani. Hiyo ni kaptura. Bila shaka, hizo ni nguo za ndani za mwanamke, na huyu hapa Adamu wake anavaa sasa. Ambapo, kulingana na Neno la asili la Mungu, "Ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi linalompasa mwanamume, na mwanamume kuvaa vazi linalompasa mwanamke," kutoka kwenye Neno la asili. Wazia jambo hilo!

72 Naam. Anazichana na kuzitia vifingirisha nywele. Baadhi ya mambo ya kuchafua moyo sana niliyowahi kuona maishani mwangu, ni baadhi ya watoto hao hapa leo wamekata nywele zao kukingama uso na kuzichana nyuma *hivi*, na nywele zilizotiwa rangi na namna fulani ya dawa ya peroksaidi, na kuitia rangi, na kuziviringisha katika vifingirisha nywele, wakizikingamisha usoni. Mwanamke mkubwa we! Hicho ni kitu kibaya sana kuzungumzia mimbarani, lakini hukumu huanzia kwenye nyumba ya Bwana. Hata hujui kama wewe ni mwanamume ama mwanamke. Nami nafahamu ya kwamba Jeshi letu la Marekani linakuja likiwa limevaa kaptura. Hiyo ni kweli. Unaona upotovu ni nini? Ni nguo za wanawake; anakata nywele kukingama uso kama mwanamke.

73 Hivi majuzi nilikuwa huko kwa Howard Johnson; si huyu aliyeko hapa, bali ni yule aliyeko kwenye

barabara ukitoka. Nami niliketi tu nyuma kwa mshangao. Huyu hapa anakuja mvulana mdogo, mdomo wazi. Na alikuwa na nywele nyeusi *hapa*, naye alizichana upande *huu*, na kuweka kifingirisha, na akazifingirisha, juu ya macho yake; akitazamia juu ya macho yake, akienda huku na huko. Kama nilipata kuona upotovu! Mnaona, asingeamini. Angeweza kuthibitisha labda alikuwa ni mwanamume, bali katika roho yake yeye ni mwanamke. Yeye hajui yuko upande gani wa nyumba. Hiyo ni kweli. Jinsi alivyopotoshwa!

Hivyo ndivyo Shetani anavyofanya. Yeye hupotosha mataifa. Yeye hupotosha kanisa. Yeye huwapotosha watu. Yeye ni mdanganyifu, mpotoshaji wa ile Kweli asili.

Mungu alimfanya mwanamume mwanamume. Alimfanya mwanamke mwanamke. Na aliwavalisha tofauti, na alimaanisha wabakie namna hiyo na kuenenda namna hiyo, mmoja ni wa kike, na mwingine ni wa kiume. Alimtenga Adamu katika Bustani ya Edeni, na akafanya hili; akamtenga Hawa kutoka kwa Adamu.

74 Sasa, yeye hukata nywele kukingamisha uso kama za mwanamke, kukata nywele zake kama za mume, na mwanamume hujaribu kuwa na nywele kama za mwanamke. Mnaona? Mwanamke huvaa nguo za mwanaume za nje, naye mwanaume huvaa nguo za mwanamke za ndani. Sasa, hilo linasikika la kukufuru, bali simaanishi hivyo. Ni Kweli ya Injili kabisa. Kama hujui, basi una kasoro; ama wewe ni kipofu ama hujawahi kuwa barabarani. Naye mwanamke na mwanamume pia hufikiria kwamba ni sahihi, wanapatana mahali fulani.

Wanawake wanasema, "Vema, kuna joto sana!"

Wazee wa Kihindi wa Apache kule wangewaaibisha. Kadiri wanavyopata joto, ndivyo wanavyovaa nguo zaidi, kujikinga na jua, kukufanya utoke jasho kusudi upate kubaridishwa wanapotembea. Mnaona? Wanasimama moja kwa moja kwenye jua.

75 Usingeweza kuvumilia cho chote; ungetokwa na malengelenge kutokana na joto kali na kuungua. Bali, mnaona, ni kile wanachoita elimu ya juu. Sayansi ya kisasa imeleta hili. Loo, jamani! Huyo hapo, "uchi" katika Laodikia, "na hajui hilo."

Alikuwa uchi huko Edeni. Mnaona hizo falme mbili zinafanana? Mmoja ni wa dhambi na kifo; ule mwingine ni Uzima na haki. Ndani humo alitiwa Utaji Mtakatifu. Wote wawili walikuwa uchi; hawakujua jambo hilo. Hawakujua kitu juu ya jambo hilo, kwa sababu walikuwa wamefunikwa na Roho wa Mungu.

Na hapa wamevaa vazi la tamaa mbaya, na wanatazamana ku… Mnaona, Adamu angeweza kumwangalia Hawa, wala hakujua alikuwa uchi. Lakini, sasa akiwa na vazi hili la tamaa mbaya, hatambui kwamba yu uchi, lakini analitenda hilo chini ya huu utaji wa tamaa mbaya kumfanya mwanamume amtazame. Ndicho kitu pekee anachoweza kufanya. Huamini jambo hilo, bali unalifanya hata hivyo, na mwanaume anaangalia. Na aliona kwamba unavutia sana, mpaka akaja na kuvaa baadhi ya nguo zako juu yake mwenyewe.

76 Loo, ni upotovu wa jinsi gani! Ni wakati ulioje! Ni wakati ulioje sisi … Jinsi lilivyo la udanganyifu! Loo, mambo haya yote, *na hajui jambo hilo,* roho iliyopotoka kabisa imo ndani ya mwanamume. Yeye ametiwa utaji kutokana na tamaa ya Shetani, na mwanamke yuko hivyo, pia. Ni roho ya kishetani ya jamii kubwa. Mnaona, hawajui, bali wao ni madhehebu. Wanawake waliovaa kaptura, ni wafuasi wa madhehebu fulani. Mwanaume aliyevaa namna hiyo, yuko kwenye dhehebu. Nitawapeni ufupi wake: C.W.W., Chama cha Wadada Wanene, kwa hiyo, wao ni wanachama wake. Wanakuja huko na chama cha wadada wanene, wakiwa na suruali ndogo, kitu kinachoonekana kichafu na cha kale chenye mafundofundo. Ni—ni …

77 Ewe Mwanamume, huenda usikubaliane nami juu ya hili, lakini huo ni Ukweli. Umekwisha potoshwa nawe hujui hilo. Wewe siyo, usitende tena kama mwanamume. Mnaona, wamekuwa wadhaifu sana, hivi karibuni hawatakuwa na cho chote ndani yao tena; wanaume, kwa wanawake, pia. Wao ni jamii. Wao ni shirika. Kwa nini? "Yohana, jirani yangu, anavaa kaptura, basi kwa nini mimi nisivae? Luella alinitaka nivae kwa sababu jirani yangu Yohana, alivaa. Na, vema, kama—kama Susie Jane anaweza kuzivaa, vivyo hivyo na Martha Jane, ama Susie Lou," ama ye yote yule, mnaona. Mnaona, ni chama. Ni shirika. Wewe ni mwanachama wake kiroho, na huna habari.

78 Na kama hilo ni kweli, na twaona ni kweli, kwa hiyo wewe umepofushwa. Umepofushwa kwa madhehebu haya ambayo Shetani amekupindapinda kwayo. Na ni upotovu wa Neno la asili la Mungu, na Ufalme Wake, na mpango Wake kwa ajili ya watoto Wake. Shetani amewapindapinda mwanaume na wanawake katika mambo haya, nao hawajui hilo. Upotovu!

Si mwana wa Mungu tena! Nywele zilizokingama uso zikining'inia usoni mwake, na kuvaa kaptura na kuzurura-zurura barabarani; mwana wa Mungu, shemasi kanisani, mchungaji mimbarani? La, huyo si mwana wa Mungu. Yeye kamwe hakupitia Chujio la kufikiri la Mungu. Asingevaa hizo nguo za wanawake, bila shaka hangalizivaa; wala yeye hangalivaa nguo za mwanamume. Mnaona, si mwana wa Mungu. Ni mwana wa Shetani, na binti wa Shetani. Ni jambo gumu kusema!

79 Shetani amefanikiwa katika kupotosha na kuuchukua ulimwengu huu, na kuufanya ufalme wake; ambamo wanadamu waliwekwa, kwa uhuru wa kuchagua, la kutenda wao wenyewe aina ya maisha waliyoyatamani. Na hiyo inaonyesha kile kilicho moyoni mwako. Mnaona? Sauti yako … Unajua nini? Matendo yako yananena kwa sauti kubwa sana, yanaizamisha sauti yako. A-ha!

Hebu niende kwa mtu fulani. Na kusema, "Loo, mimi … Sisi sote ni Wakristo. Sisi ni wafuasi wa kanisa." Na picha za wanawake walio uchi zikining'inia kila mahali ofisini mwake? A-ha! Atakachoniambia hakitaleta tofauti, ningejua bora zaidi; na wewe pia.

Kuacha mwanamke asema yeye ni Mkristo, akiwa na nywele fupi? A-ha! Mnajua vizuri zaidi ya hayo, mnaona. Naam, bwana. Hebu na aseme yeye ni Mkristo akiwa amejipaka rangi na poda, na kaptura, na kusema ni Mkristo? Mnajua vizuri zaidi ya hayo. Neno la Mungu linakufundisha vizuri zaidi ya hilo. Neno linasema hawezi kufanya hivyo na kuwa Mkristo. Yeye hata hana heshima, na kila kitu. Mungu atawekaje kitu cha aibu katika Ufalme Wake? La, bwana, hata kidogo. La, bwana. Wenyewe, wanaonyesha shauku yao.

80 Huwezi kumpa hua kula na mwewe, hata kidogo. Hua hana nyongo yo yote. Hawezi kula mzoga huo uliooza. Kama akiudonoa mara moja, ungelimuua, naye anajua hivyo. Lakini mwewe anaweza kula karibu cho chote anachotaka kula. Mnaona? Yeye ana nyongo nyingi.

Kwa hiyo basi mnaona, hivyo ndivyo ilivyo na ulimwengu siku hizi, jambo lile lile, "Wao ni uchi, vipofu, wala hawajui."

81 Shetani alifanya hivyo kwa tamaa ya mwanamke ya kupata maarifa, ya kujuana kimwili, ambayo alijichagulia mwenyewe. Sasa angalia, Hawa ndiye aliyemwongoza Adamu kwenye makosa, na mwanamke ndiye aliyevua nguo zake kabla Adamu hajavua zake. Mnaona? Ni mwanamke, daima. Imekuwa hivyo daima. Bado ni vivyo hivyo.

Kanisa ndilo linalompoteza mwanadamu. Ni kanisa, mnaona, linalomwongoza mtu aliyetaka kuwa mwana wa Mungu. Ni mwanamke, kanisa. Si Biblia, Mungu, kwa kuwa Biblia ni mwanadamu. Loo, naam, "Neno lilifanyika mwili," Naye alikuwa Mwanadamu. Mnaona? Biblia ni mwanadamu; kanisa ni mwanamke. Mnaona? Si kanisa … Biblia ndiyo inayompoteza mtu. Kanisa ndilo linalompoteza. Ni kanisa aliloenda nalo uchi, si Biblia. Mnaona? La, hapana. Biblia inamwambia yu uchi. Naam, bwana.

Sasa angalia jinsi, kwa kujuana kimwili, tamaa ya kujuana kimwili, yeye alitamani maarifa, kujua ni kitu gani *hiki*, na jinsi gani, kama tunda hili lilikuwa zuri au la. Naye akafanya hivyo.

82 Mungu ataurudisha hata hivyo siku fulani, kwa mwanamume. Ulitolewa na mwanamke. Lakini ulikombolewa na mwanamume, mwanamume, Yesu Kristo, ambaye ni Neno.

Halafu basi ni kitu gani? Angalia, katika kufunga. Hapa si muda mrefu uliopita, nilitoa tamshi hili. Nina kama kurasa nne ama tano zaidi mle ndani, lakini mimi … ya Maandiko na mambo niliyotaka kuyarejea. Lakini, sikilizeni. Hebu tufunge, katika kusema jambo hili.

83 Kumbukeni, hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikiwafundisha juu ya zile Baragumu Saba, *Sikukuu ya Baragumu*, na kadhalika. Nami nikasema, "Kuna sikukuu ya siku ya nane." Kwa hiyo, siku ya saba ingekuwa ndiyo ya mwisho, huo ungekuwa ni ule Utawala wa Miaka Elfu. Lakini kuna sikukuu ya siku ya nane; ambayo, kama ilikuwa ni ya nane, na kuna siku saba tu, ingeifanya siku ya kwanza tena, kurudi moja kwa moja kwenye siku ya kwanza. Ndipo, baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu kumalizika, basi kutakuwako na Edeni iliyosimikwa tena. Ufalme mkuu wa Mungu utarudishwa. Kwa sababu Yesu aliupigania dhidi ya Shetani, katika Bustani ya Gethesemane, na akainyakua Edeni; ambayo, amekwenda kuiandaa huko Mbinguni kurudi tena, huko Mbinguni. Yeye alisema, "Msifadhaike mioyoni mwenu."

84 Wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, "Ninyi, ninyi Wayahudi, mmemwamini Mungu. Sasa, ninajua nina jina baya,"Yeye alisema. "Nao wanasema mimi ni *huyu*, yule *mwingine*. Lakini, mmemwamini Mungu; na kwa kuwa mmemwamini Mungu, niaminini na Mimi." Yeye alikuwa Mungu, aliyedhihirishwa. Mnaona? "Amini pia katika …"

85 "Nyumbani mwa Baba Yangu mna mengi …" Ama, "Katika uchumi wa Baba Yangu, katika mipango ya Baba Yangu kuna majumba mengi ya kifalme. Nitaenda kuandalia mahali." Angalia jinsi yalivyo marefu—maili 1500 mraba. Aisee, yako wapi? Ameenda kuitayarisha. Yeye ni Muumba. Yeye huumba dhahabu hiyo yote. Barabara Zake zinaona kama kioo. Yeye ni Muumba. Yeye anatengeneza mahali. Katika Ufunuo 21, alisema, "Nami, Yohana, niliona Mji ule Mtakatifu, Yerusalemu Mpya ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu."

"Hakukuwa na bahari tena; mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza zilipita." Mbingu zetu za kwanza zilikuwa nini? Ulikuwa ni ule Utawala wa Miaka Elfu. Nchi ya kwanza ni nini? Ilikuwa hii. Itafanywa upya. Kama tu ilivyobatizwa na Nuhu, katika siku za kuhubiri kwake; ilitakaswa na Kristo alipoinyunyizia Damu Yake, na kufanywa upya, kuondoa wadudu wote wabaya na kila kitu juu yake, katika kuifanya upya hapo

mwishoni, kwa ubatizo wa moto ambao utaua kila mdudu mbaya, kila maradhi, kila ugonjwa, kila uchafu uliowahi kuwa duniani.

86 Dunia itapasuka, na kuwa dunia mpya. "Nami nikaona Mbingu Mpya na Nchi Mpya. Mbingu za kwanza na nchi za kwanza zimekwisha pita, na hapakuwa na bahari tena. Nami Yohana nikauona Mji ule mtakatifu, Yerusalemu Mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu Mbinguni." Hapo Mungu atakuwa pamoja na sifa Zake za kweli, wana na binti, ambapo Yeye anaweza kushirikiana nao katika utakatifu, huku macho yao yamepofushwa kwa dhambi yoyote. Hakutakuwako na dhambi tena tangu hapo na kuendelea.

Hebu na tujitahidi sana; msidanganyike katika siku hii, bali, "jitahidini kuingia mlangoni."

"Kwani wote watakaoachwa nje, watakuwa wazinzi, wenye tamaa mbaya." "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye." Wote pamoja—huko nje watakuweko wanawake wenye sifa mbaya, mwanaume mwenye sifa mbaya, na kadhalika,

Na ni wale tu waliokombolewa, na walio katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo wataingia mlangoni. Kwa hiyo jitahidini, marafiki; msidanganywe katika siku hii ya mwisho.

87 Huu ni wakati mkuu sana. Kila mtu ana pesa. Kila mtu anaweza kufanya jambo *hili*, na kila mtu anaweza kufanya jambo *hilo*, na pesa zinapita kila upande, na magari makubwa, na kila kitu. Hakutakuwa na mmoja wao katika Mji huo. Hakutakuwako na gari moja, ndege moja. La. Utakuwa ni ustaarabu tofauti kabisa. Utakuwa ni ustaarabu tena si wa maarifa, si wa sayansi, bali wa kutokuwa na hatia, na imani katika Mungu aliye hai.

Hebu na tujitahidi kuingia katika Huo. Kwani hilo ndilo kusudi langu lote, ni kuingia katika Mji ule siku moja, na angalia nyuma tu, njoo pamoja nami, uone kila mmoja wenu akipiga hatua taratibu, tutakapoimba, "Watakatifu wakiingia taratibu. Nataka kuwa katika hesabu ile, watakatifu watakapokuwa wakiingia taratibu."

Hebu na tuombe.

88 Baba mpenzi wa Mbinguni, siku zinapokaribia kwisha, na twaona hilo linakaribia, ile ahadi inakaribia. Tunaomba, Mungu Mpendwa, ya kwamba utaweka hilo juu ya mioyo yetu, ili tusifanye kosa lo lote. Mungu mpendwa, dumisha dhamiri zetu. Ifunike mioyo yetu, Bwana, macho yetu yafunikwe yasione mambo ya ulimwengu, na mambo yasiyo na maana ya ulimwengu, utukufu usio na maana wa kufanywa mtu mkubwa fulani.

Haidhuru ni wakubwa kiasi gani, wafalme wote, wenye mamlaka, wenye nguvu, na kila kitu kingine lazima kiangamie, nao hawatafufuka katika wa wapil ... katika ufufuo wa kwanza. Kwa maana imeandikwa, "Heri na mtakatifu ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza, ambao juu yake mauti ya pili haina nguvu." Ee Mungu! "Mauti ya pili," mauti ya kiroho, "haina nguvu"; amekombolewa!

89 Ee Mungu, kuwazia ya kwamba moja ya saa hizi, mmoja ataenda kumtembelea mwingine, na kunyakuliwa. "Wawili kitandani, nitamchukua mmoja, na kumwacha mmoja. Wawili kondeni, nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja."

Ee Mungu, tusaidie kuwa safi katika—mbele Zako, Bwana, haidhuru mwanadamu atafikiria nini juu yetu, kile watu wengine husema, Bwana, hebu utakatifu wetu…mazungumzo yetu yawe matakatifu. Hebu yakolee Neno la Mungu; yakolee sana, Bwana, hata halitaonekana waa ndani yetu. Wakati tunaposihi, katika makosa yetu yote, kwamba Damu ya Yesu Kristo itasimama kati yetu na Mungu, kwamba atatuangalia kupitia Damu ya Yesu. Si juu ya haki yetu, au eti sisi ni akina nani, au tulilotenda, bali katika fadhili Zake pekee. Mungu, jalia hilo!

90 Jalia kusiwe na mtu yeyote anayeketi hapa usiku wa leo na kuusikia Ujumbe, jalia hata mmoja wao asipotee, kutoka kwa mtoto aliye mdogo kuliko wote hadi kwa mtu aliye mkubwa kuliko wote. Jalia shauku yao takatifu iwe tu kwa ajili ya Mungu na Neno Lake. Hatujui ni saa gani anayoweza kuonekana, ama ni saa gani anayoweza kutuita kujibu kule kwenye Hukumu. Hatujui ni saa gani Yeye anaweza kutuita, kama ilivyokuwa, kuchukua kadi yetu kutoka kwenye chombo cha kadi, aseme, "Ni wakati wa kurudi nyumbani. Huna budi kuondoka." Mungu, tusaidie tuwe safi. Jalia hilo, Bwana.

Jalia tuishi mpaka Kuja kwa Bwana, ikiwezekana. Jalia tufanye kila kitu kilicho katika nguvu zetu, kwa upendo na ufahamu, tukifahamu ya kwamba Mungu anauchunguza ulimwengu, leo, akimpata kila kondoo aliyepotea. Na jalia tuzungumze nao kwa maombi ya majira ya upendo na Neno la Mungu, ili tupate hilo la mwisho, ili tuweze kwenda Nyumbani, na kutoka katika Edeni hii ya kale ya Shetani hapa, Bwana.

91 Hiyo yote imejengwa juu ya tamaa mbaya, na wanawake wanaojiita warembo ulimwenguni, kwa matangazo yao huko, "Tunatangaza, na tunataka wavulana waje wakiwa na jamu kwenye nyuso zao, na wasichana warembo wamevaa kaptura," moja kwa moja kwenye redio na televisheni; na kila namna ya uchafu na unajisi, na Hollywood; kila aina ya mavazi ya wanawake ya kinajisi, machafu, na takataka. Na

—na wanaume wakiwa wamepotoka na wakivaa mavazi ya wanawake, na kukata nywele zao kama wanawake; na wanawake kama wanaume.

Ee Mungu, ni saa ya kuchukiza iliyoje tunayoishi! Loo, njoo, Bwana Yesu, njoo! Njoo, Bwana! Tusafishe kwa Damu. Tuondolee uchafu wote na hila. Jalia tuishi, Bwana, jalia tuishi chini ya Damu, daima, mbele Zako. Ni shauku ya mioyo yetu, na ombi letu la kweli.

92 Mungu mpendwa, ukiwa kwenye hii—au hizo, dawati, usiku wa leo, ambapo Injili imewekwa. Bwana, hapa kuna leso na vifurushi vidogo vinavyowaendea wagonjwa na wanaoteseka. Jalia maombi ya imani, Bwana, yashuke kutoka mioyoni mwetu sasa, machoni Pako. Basi, Bwana, kama kuna kitu chochote kichafu ndani yetu, Bwana, tuchukue … tupeleke hukumuni sasa; nasi tunaomba rehema. Tufunulie kile tunachokosea, Bwana, ili tuweze kuomba, kuichukua Damu na kutusafisha. Waponye watu hawa wagonjwa na uwafanye wazima, Baba, cho chote kiendacho, po pote waendako. Waponye watu hawa wagonjwa, na uwape afya, Baba, ko kote inakoelekea; ko kote waendako. Jalia iwe hivyo, Baba.

93 Tupe dhamira ya kukutumikia Wewe, na Wewe tu. Jalia hilo, Bwana.

Wape usalama watu hawa wapendwa walio njiani kuelekea nyumbani.

Asante kwa jinsi ulivyowaponya watu. Na mvulana mdogo wa Dada Shepherd na Ndugu Shepherd, aliyeumia kwenye baiskeli, naomba kwamba uovu wowote usimfikie; jamaa huyo mdogo akiendesha baiskeli yake, naomba kwamba atakuwa mzima. Tunakushukuru kwa ajili ya uponyaji Wako kwa hawa wengine ambao tumewaombea. "Nasi tunajua ya kwamba tuombalo, tunapokea, kwa sababu tunamtumaini Yeye aliyetoa ahadi."

Tupe neema Yako, Bwana, na utusamehe dhambi zetu, tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

94 Je! Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mnamwamini? ["Amina."] Je, wewe ni mgonjwa na umechoshwa na ufalme wa Shetani? ["Amina."] Je! Unaamini unakuja kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, kwenye ule Utawala Wake wa Miaka Elfu; Yake, kwa Edeni Yake? ["Amina."]

Unaamini imeumbika leo? Angalieni, kila kitu kina msingi wa wasomi. Yote, kila kitu, hayana budi kuthibitishwa kisayansi kabla hawajaamini.

Wala huwezi kumthibitisha Mungu kisayansi. Inakubidi kumkubali kwa imani, "Kwa maana yeye amjiaye Mungu hana budi kuamini ya kwamba Yeye yuko, na huwapa thawabu wale wamtafutao."

Ee Mungu, sitaki kujua kitu ila Damu ya Yesu Kristo inayonitakasa dhambi. Sijui kitu ila Yesu Kristo. Na kama vile Paulo alivyosema zamani, ndivyo ninavyosema usiku wa leo, "Sijui neno miongoni mwenu, ila Yesu Kristo, Naye amesulibishwa."

95 Hayo tu ndiyo ninayojua kuwaambia. Kwamba, Biblia hii, ninaamini kwa moyo wangu wote (kama ninajua moyo wangu), kuwa Neno kamili la Mungu lisiloghoshiwa. Kwa Hili naishi. Kwa Hili ninasimama. Na kama ningalikuwa na maisha elfu kumi, ningetaka kutoa kila sehemu yake kwa ajili ya Neno hili, kwa kuwa ni Neno la Yesu Kristo. Nami sijali ni kiasi gani wanaweza kujaribu kukanusha jambo Hilo, ni kiasi gani sayansi inajaribu kusema Hilo haliaminiki, na kadhalika. Kwangu mimi, ndicho kitu pekee ulimwenguni ninachoweza kuamini, ni Neno hili. Yeye ni wangu. Ninampenda. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

96 Kama kuna dhambi moyoni mwako, kama kuna kosa moyoni mwako, kama una cho chote, omba sasa na umwombe Mungu akusamehe. Wewe niombee; Nitawaombea. Mungu akubariki, ndilo ombi langu.

> Hata tuonane! hata tuonane!
> Mungu awe nanyi mpaka tuonanapo!

Je! Mnapendana? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Yohana alisema, "Watoto wadogo, pendaneni." "Pendaneni, kwa maana upendo hufunika dhambi nyingi." Sasa hebu na tupeane mikono sisi kwa sisi.

> Mungu awe nanyi mpaka tuonanapo!
> Hata tuonane! hata tuonane!

Sasa iweni wenye fadhili ninyi kwa ninyi. Uwe mwema kwa kila mtu. Mtendee jirani yako kwa usahihi. Jiweke bila waa hadi Yesu atakapokuja.

> … miguu;
> Hata tuonane! hata tuonane!
> Mungu awe nanyi mapaka tuonanapo!

97 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hayo ndiyo maombi yangu. Ninyi niombee; Nitawaombea. Sina budi kurudi Tucson sasa. Nami na—naomba ya kwamba Mungu atawabariki ninyi nyote. Ninaenda kutoka huko kwenda Canada, na kurudi Colorado; kuzunguka, kuzunguka, kuzunguka, mnaona. Mpaka …

Ndugu Tony yuko kule, na jambo kubwa limetukia. Moja kwa moja chini ya Vatican, huko Rumi, wanaitisha ufufuo, mkutano, nije kule na kufanya uamsho huko Rumi, huko Rumi. Yeye alirudi tu. Watu wote wako pamoja. Wana uwanja mkubwa pale, wanapoketi maelfu na maelfu, nao wanataka nije kwa ajili ya uamsho. Wanataka kuona utukufu wa Bwana katika huduma. Sijui. Sina budi kuliombea, kuona yale Bwana atakayoniambia. Loo, jamani! Kumbukeni, tuombeni, sisi sote pamoja. Tunafanya kazi …

Tunatazamia kule kuja kwa Mwokozi wetu aliyebarikiwa,
Loo, na angalia majani ya mtini sasa yakiwa kijani,;
Injili ya Ufalme Wake imekwenda kwa kila taifa;
Na ni dhahiri tumekaribia mwisho, inaweza kuonekana.

Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Na kwa furaha hebu tupige mbiu ya ujumbe wa kufunuliwa Kwake kubarikiwa.
Hivi karibuni Yeye anakuja katika utukufu, kila mmoja na ajulishwe;
Basi amkeni, enyi watakatifu wa Bwana, kwani mlale wakati mwisho unakaribia,
Hebu na tuwe tayari kwa ajili ya wito huo wa mwisho.

98 Atageukia magharibi na kurudi tena, moja ya siku hizi, kumbukeni tu. Hakika atafanya hivyo. Na hiyo ni kweli. Mpaka wakati huo:

Peleka Jina la Yesu,
Mwana wa huzuni na shida;
LItakupa furaha na faraja,
Lipeleke, popote uendapo.
Jina la thamani (Jina la thamani), Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje! (jinsi lilivyo tamu!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.
Tukiinama mbele ya Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Mfalme wa wafalme Mbinguni tutamvalisha taji,
Wakati safari yetu itakapokamilika.
Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la dunia na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la dunia na furaha ya Mbinguni.

99 Sasa, kwenye aya hii ya mwisho, hebu na tuuimbe kwa mioyo iliyoinamishwa sasa.

Peleka Jina la Yesu,
Akiwa ngao toka kwa kila mtego;
Majaribu yanapotuzunguka, (mambo haya ya ufalme wa Shetani, mnaona, mnaona)
Upumue tu Jina hilo katika maombi.

Hivyo tu; kisha ondoka. Linatenda kazi. Nimejaribu hilo. Hebu liamini tu sasa, maana litafanya kazi. Pumua tu Jina Lake takatifu katika maombi.

… Jina la Yesu pamoja nawe,
Kama ngao kwa kila mtego;
Unapozungukwa na majaribu yakikuzunguka, (Unafanya nini basi?)
Tamka tu Jina hilo Jina takatifu katika maombi. (Pazia litakuja juu ya uso wako wakati huo.)
Jina la thamani (Jina la thamani), Ee ni zuri jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbingu;
Jina la thamani, O ni zuri jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbingu.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, ninapomwomba Ndugu Beeler kule nyuma aje hapa jukwaani. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha Peleka Jina La Yesu — Mh.]

Lipumue tu Jina Lake takatifu katika maombi.

Turyhysu tuondoke, Ndugu Beeler. Turuhusu katika maombi.

Jina la thamani,
Tumaini la dunia na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani (Jina la thamani), Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la dunia na furaha ya Mbinguni.

100 Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na mioyo yetu imeinamishwa. Ndugu Beeler, mmoja wa washiriki wetu hapa, Ndugu Estle Beeler, ndugu mzuri Mkristo, mtu mwaminifu. Nitamuuliza kama atawaruhusu watu waondoke, usiku wa leo, kwa maombi. Mungu akubariki, Ndugu Beeler.

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7